Nuru ya Kiswahili, Juzuu 2(2), Desemba 2023: 1 - 24

# Mtazamo kuhusu Wakati katika Falsafa ya Kiafrika: Mifano kutoka Riwaya Teule za Kiswahili

**Stella Faustine**
**Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Dodoma**

stelafau@gmail.com

**Ikisiri**
Waafrika kama zilivyo jamii nyinginezo duniani wana falsafa inayoongoza maisha yao. Katika uga wa fasihi, wataalamu mbalimbali wametafiti na kuangalia namna falsafa hiyo inavyodhihirika kupitia vipengele mbalimbali vya maisha. Hata hivyo, mtazamo kuhusu wakati kama kipengele kinachoibua Falsafa ya Waafrika, kwa kuhusisha udhihirikaji wake na vipengele vingine vya kifalsafa hakijamakinikiwa vya kutosha. Jambo hili linasababisha ufinyu wa mawanda katika kuelewa mtazamo wa falsafa ya wakati, uhusiano wake na vipengele vingine vya kifalsafa pamoja na athari zake kwa jamii ya Waafrika. Kwa kuzingatia pengo hilo la kimaarifa, makala hii imekusudiwa kubainisha mtazamo kuhusu wakati kwa Waafrika kama unavyodhihirika kupitia vipengele mbalimbali vya kifalsafa pamoja na athari zake kwa jamii. Data za makala hii zilikusanywa maktabani na uwandani. Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika ilitumika katika uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Kwa ujumla, makala inabainisha kuwa mtazamo kuhusu wakati ni kipengele muhimu sana kwa Waafrika kwani una athari kubwa kwa namna wanavyoyaendesha maisha yao. Waafrika wanaamini kuwa wakati ni kiini cha 'kuwapo' kwa mwanadamu kunakojibainisha kupitia vipengele mbalimbali katika maisha kama vile uzazi, maisha baada ya kifo pamoja na busara na hekima ambazo huaminika kuwapo kwa wazee walio hai pamoja na waliokufa.

**Dhana za Msingi:** Falsafa, Falsafa ya Kiafrika, Riwaya, Wakati

## Utangulizi

Waafrika, kama jamii nyinginezo duniani, hufungamanishwa na misingi ya falsafa yao ambayo ina athari kubwa kwa namna wanavyoutafakari na kuupa maana ulimwengu wanaoishi (Tempels, 1969; Mbiti, 2011; Chuachua, 2016; na Faustine, 2017). Kimsingi, falsafa hiyo hujibainisha katika vipengele mbalimbali vya maisha. Vipengele hivyo ni usadikifu wa kuwapo kwa nguvu hai ambayo hufanya kazi kwa mfumo wa kidarajia kuanzia kwa Mwenyezi Mungu – wahenga – mababu – wazazi na hatimaye hushuka kwa watoto (Tempels, 1969 na Faustine, 2017). Pia, kuna dhana ya familia pana ambayo hujumuisha waishio na waliofariki (Tempels, 1969; Mbiti, 2010; na Kajosi, 2013). Vipengele vingine vinavyoijenga Falsafa ya Kiafrika ni kuwapo kwa ulimwengu wa matabaka matatu ambayo ni duniani wanakoishi viumbe hai, kuzimu wanakoishi wafu, na mbinguni ambako ndiko anakoishi Mungu Mkuu (Tempels, 1969 na Mbiti, 2011). Pia, kuna suala la uzazi kama njia ya mwendelezo wa duru ya maisha (Magesa, 1998), umuhimu wa malezi kama sehemu ya kujenga maadili na maandalizi ya mwanadamu katika kuukabili ulimwengu wake (Faustine, 2017), pamoja na dhana ya uhai na kifo (Tempels, 1969 na Mbiti, 2011). Zaidi, falsafa hiyo hujibainisha kupitia usadikifu wa kuwapo kwa hekima na busara kwa wazee wenye umri mkubwa; hapa hujumuishwa walio hai, pamoja na wafu hai (wahenga) ambao husadikiwa kuwa wana maisha mengine katika ulimwengu wa wafu (Tempels, 1969), kuwapo kwa uchawi na dhana ya uduara (Tempels, 1969 na Faustine, 2017).

Kipengele kingine ambacho kimetazamwa na wataalamu mbalimbali kama sehemu ya kuibua maarifa ya kifalsafa kwa jamii ya Waafrika ni dhana ya wakati. Miongoni mwa wataalamu waliojadili kipengele hiki ni Mbiti

(2011). Huku akirejelea mifano kutoka jamii ya Wakamba, mwanafalsafa huyu anafafanua mambo kadhaa yanayobainisha namna Waafrika wanavyoutazama wakati kwa kuuhusisha na namna wanavyoyaendesha maisha yao. Kwanza, anaeleza kuwa kwa Waafrika, wakati haupotei bali huzalishwa. Hii ina maana kuwa mtu anapochelewa au kushindwa kufanya jambo kwa wakati fulani na kutumia wakati huo kufanya jambo jingine hakupoteza wakati, bali anakuwa amezalisha wakati kwa kufanya jambo lingine.

Pili, ni usadikifu kuwa dhana ya wakati kwa Waafrika hupimwa katika utimilifu wa matukio yaliyokwishatokea (wakati uliopita) na yanayotokea (wakati uliopo – sasa). Mbiti (2011) anatoa majumuisho kuhusu dhana ya wakati kwa Waafrika kwa kuirejelea jamii ya Wakamba kuwa inautazama wakati katika ncha mbili ambazo ni zamani na sasa. Hii ni kwa sababu ni katika zamani na sasa ambapo kuna utimilifu wa matukio. Kutokana na mawazo ya Mbiti (2011), Waafrika hawana matarajio yao katika kesho kwa sababu matukio yatarajiwayo huwa ni dhahania na si timilifu. Kwa hiyo, hawana cha kufikiria katika kesho itarajiwayo. Kwa Waafrika, zamani na sasa havitengamani hivyo, kuwapo kwa wakati mmoja (sasa) kunategemea kuwapo kwa wakati uliopita (zamani).

Mawazo ya Mbiti (2011) yamekuwa chachu ya kufanyika kwa tafiti nyingi kuhusu Falsafa ya Kiafrika. Miongoni mwa tafiti hizo ni zile zinazoupinga mtazamo wa Mbiti (2011) kuwa Waafrika wanaishi kwa kuutazama wakati katika ncha mbili, na hivyo, hawana kesho. Kwa mfano, Gyekye (1995) anathibitisha kuwa maisha ya Waafrika hayajakitwa katika zamani na sasa tu kama inavyoelezwa na Mbiti (2011), bali pia katika kesho itarajiwayo. Anathibitisha hili kwa kutoa ufafanuzi kuwa, katika asili, jamii ya Waakan

ilikuwa na kalenda yake (*Akusikan Calender*) ambayo ilibainisha matukio mbalimbali yaliyotarajiwa kutokea. Anaendelea kubainisha kuwa, kwa Waafrika, wakati ni dhana inayojumuisha mabadiliko, mchakato na tukio husika, na kila kimoja katika kutokea kwake, hakina athari katika suala zima la wakati. Gyekye (1995) anaeleza pia kuhusu fikra za Waafrika za kuyatazamia mambo katika ncha tatu kupitia lugha ya Kiakan. Anasema kuwa katika lugha ya Kiakan, muundo wa sentensi umekitwa katika nyakati tatu, yaani wakati uliopita, uliopo, na ujao. Mawazo haya yanashabihiana na yale yanayotolewa na Babalola na Alokan (2013) kuwa kila jamii ina namna yake ya kulitazama suala la wakati. Anafafanua kuwa Waafrika kuutazama wakati kwa kuirejelea zamani ni sehemu ya utambulisho wao ambao pia, umeifumbata historia na maarifa ya kifalsafa ya jamii hiyo. Babalola na Alokan (2013) wanatoa mfano kwa namna Waafrika wanavyoutazama muda kupitia falsafa ya maisha baada ya kifo kama inavyotazamiwa na jamii ya Wayoruba. Kimsingi, mawazo ya Babalola na Alokan (*wameshatajwa*) kuhusu falsafa ya maisha baada ya kifo, yanajenga picha kwa namna Waafrika wanavyoutazama muda kwa kuumulika katika umbali mrefu wa wakati utarajiwao. Aidha, wataalamu hawa wanatoa majumuisho yanayolandana na yale yanayotolewa na Nnajiofor (2016) kuwa Waafrika wanautazama wakati kama tukio linaloambatana na utamaduni wa jamii husika. Wanathibitisha kuwa Waafrika kuufungamanisha muda na matukio ya kijamii, haimaanishi kuwa hawaitazamii kesho yao.

Kezilahabi (2006) ameijadili dhana ya wakati kwa kuihusisha na utandawazi katika mitazamo minne akiziambatanisha na suala la kuwako kwa vyote vilivyomo ulimwenguni. Nazo ni wakati katika dhana ya mstari

sambamba ambayo inauhusisha wakati na suala la maendeleo. Nyingine, ni dhana ya mviringo ambayo huuweka wakati kama kitu kisichosonga mbele na hubaki palepale daima kwa kujirudia. Anabainisha kuwa dhana ya mviringo hudhihirika zaidi katika misingi ya utoaji majina ya urithi. Pia, amejadili dhana ya udhanaishi (maana ya maisha) inayozua suala la kuwako. Mwisho, ni dhana ya mabadiliko ambayo inahusishwa na kuwako kwa neno kwanza kabla ya mabadiliko yenyewe. Kezilahabi (2006) anazishikamanisha hoja zake na suala la wakati kwa kusema kuwa wakati ni kipimo cha maisha. Hakuna kinachoweza kutokea nje ya wakati. Katika muktadha huu, inahalisika kusema kuwa maisha ya Mwafrika yanaamuliwa na misingi ya kiwakati. Vipengele vya kitamaduni, historia, na falsafa vimefungwa katika kapu kubwa la wakati.

Marava (2015) ameitazama dhana ya muda kwa kuihusisha na falsafa ya maisha baada ya kifo kwa kadri ya mtazamo wa Wazimbabwe. Hoja za msingi anazozimakinikia katika utafiti wake zinatokana na maswali kuwa: Je, maisha ya mwanadamu yanakoma mara tu baada ya kifo chake? Je, wafu wana mawasiliano yoyote na walio hai? Na je, kifo ni mwanzo wa maisha mengine kwa kadri ya mtazamo wa Wazimbabwe? Maswali haya yamejengwa katika muktadha wa kulitazama suala la wakati kwa kulihusianisha na dhana ya kifo na maisha baada ya kifo kwa mwanadamu. Anahitimisha kwa kusema kuwa wakati ni suala la msingi sana katika kuangazia mtazamo wa jamii mbalimbali kuhusu suala la kifo na maisha baada ya kifo. Anatoa mapendekezo ya kufanyika kwa tafiti nyingi zaidi ili kupanua wigo wa kimaarifa kuhusu uhusiano wa suala la wakati na maisha baada ya kifo kwani, katika utafiti wake, amegundua kuwapo kwa

mitazamo kinzani kuhusu suala hilo, hasa kutokana na kuwapo kwa imani tofauti pamoja na utofauti wa kimaeneo.

Aidha, mijadala ya wataalamu mbalimbali waliorejelewa katika sehemu hii kuhusu dhana ya wakati ilikuwa ni kichokoo kikubwa cha kufanyika kwa utafiti uliozalisha makala. Hii ni kwa sababu, mijadala hiyo ilipanua wigo wa kimaarifa kuhusu namna dhana ya wakati inavyodhihirika kupitia mambo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii ya Waafrika ambayo ni: Kwanza, lugha za jamii husika (Gyekye, 1995 na Nnajiafor, 2016). Pili, ni dhana ya uhai na kifo ambayo inafafanuliwa na Babalola & Alokan (2013) na Marava (2015). Hawa, wameonesha kwa jumla sana namna dhana ya kifo na maisha inavyobainisha namna Waafrika wanavyoutazama muda kwa kuhusisha na matumaini ya kuwapo kwa maisha mengine baada ya kifo. Tatu, ni mtazamo unaotolewa na Nnajiofor (2016) kuwa dhana ya wakati kwa Waafrika inadhihirika kupitia uzoefu alionao mtu, matukio yanayojitokeza katika jamii pamoja na shughuli mbalimbali zinazoizunguka jamii. Kimsingi, hoja za wataalamu hawa kuhusu namna Waafrika wanavyolitazama suala la wakati, ndizo zilizotoa msukumo wa kufanyika kwa utafiti huu ambao umepanua mawanda ya mjadala kwa kuangalia namna dhana ya wakati inavyoweza kutazamwa kupitia vipengele mbalimbali vya falsafa kama vinavyojitokeza katika kazi za fasihi, pamoja na athari za mtazamo huo kwa jamii ya Waafrika. Vipengele vilivyomakinikiwa katika mjadala wa makala hii ni vinne ambavyo ni uzazi kama jambo muhimu na lenye thamani kwa Waafrika, malezi kama msingi wa maadili kwa jamii, uhai na kifo kama kipengele muhimu katika kuendeleza duru ya maisha, pamoja na busara na hekima kama msingi wa maadili kwa jamii.

**Muhtasari wa Riwaya Teule**

Kwa mujibu wa Faustine (2017), riwaya za *Bina – Adamu! Babu Alipofufuka* na *Nagona* ni za kisasa ambazo zinawekwa katika mkondo wa riwaya za kimajaribio. Waandishi wa riwaya hizi wametumia mtindo wa uhalisiajabu katika kuwasilisha maudhui yao. Riwaya ya *Bina – Adamu!* ilitungwa na K. W. Wamitila na kuchapishwa mwaka 2002. Mwandishi anatumia taswira na ishara mbalimbali zilizofumbatwa katika sitiari kuu ya kijiji sambamba na safari ya Bina Adamu Msafiri kueleza madhila yanayozikumba nchi zinazoendelea; kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi. Riwaya ya *Babu Alipofufuka* imetungwa na S. A. Mohamed na kuchapishwa mwaka 2001. Katika riwaya hii, mwandishi anajadili matatizo yanayoukabili ulimwengu kisiasa, kiuchumi, na kiutamaduni. Hoja muhimu ambayo inaibuliwa na mwandishi sambamba na kujadili matatizo hayo ni suala la kuwapo kwa mwanadamu, kutokuwapo kwake, uhusiano wake na watu pamoja na vitu vingine katika ulimwengu anamoishi. Kwa kutumia mtindo wa uhalisiajabu, anaiwasilisha falsafa pana ya Waafrika kuhusu suala la maisha kuwa tupo, hatufi bali tunapita katika ulimwengu tuliomo kuelekea katika ulimwengu usioonekana wanakoishi wafu hai. *Nagona* ni riwaya iliyotungwa na E. Kezilahabi na kuchapishwa mwaka 1990. Mwandishi anatumia mtindo wa uhalisiajabu kubainisha mtazamo wake kuhusu maisha. Ndani yake, anaibua kitendawili kinachomtaka msomaji kutafakari maisha ni nini, yana thamani gani na mwisho wake ni nini. Aidha, anajenga tafakuri hiyo kwa kutumia dhihaka, kejeli, taswira, ishara na mafumbo ambayo ndani yake ndimo jibu la fumbo kuu kuhusu maisha linamopatikana.

## Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Reeve (2016) anafafanua kuwa Nadharia ya Ontolojia iliasisiwa na mwanafalsafa Aristotle alipokuwa anafafanua mambo yanayohusiana na Metafizikia. Kwa mujibu wa Reeve, Aristotle aliona kuwa Ontolojia kama nadharia, msingi wake mkuu umeegemea katika namna ya kushughulika na kuwapo kwa vitu na kategoria zake. Wataalamu wengine walioeleza kuhusu Nadharia ya Ontolojia ni Perrinder (1962), Coffey (1918), Carazzon (2010) na Mbiti (2011), wakitajwa baadhi tu. Kwa ujumla, mawazo yao yanabainisha misingi ya Nadharia ya Ontolojia ambapo miongoni mwa misingi hiyo, mitatu ndiyo iliyotumika katika uchambuzi na uwasilishaji wa data. Msingi wa kwanza ni dhana ya kuwapo kwa kitu katika dunia (Wolff, 1962 na Mbiti, 2011). Wolff (1962) anafafanua kuwa kuwapo kunaelezwa katika wakati uliopita na ujao, yaani, vilivyopo na vitarajiwavyo, yaani kuwapo kunajibainisha katika vipengele mbalimbali ambavyo vina sifa ya kutambuana na kuathiriana. Katika mjadala wa makala hii, msingi huu umetumika kubaini vipengele mbalimbali vya falsafa vinavyohusiana na kuwapo kwa mwanadamu ambavyo ni uzazi, malezi, uhai na kifo pamoja na busara na hekima (Mbiti, 2011; Faustine, 2017 na Kaponda, 2018). Msingi wa pili ni kuwapo kwa kategoria na mahusiano ya kategoria hizo (Wolff, 1962). Msingi huu ulitoa mwongozo kubaini mahusiano ya vipengele mbalimbali vinavyohusiana na kuwako kwa Mwafrika na mtazamo kuhusu suala la wakati. Tatu, ni msingi kuwa Ontolojia ni zao la muda mrefu linalotokana na uzoefu walionao watu pamoja na hisi (Kant, 1998). Msingi huu umesaidia kuelewa mahusiano ya vipengele mbalimbali vinayobainisha kuwapo kwa mwanadamu, hususani kwa kuhusianisha na tajriba ya maisha

ya Mwafrika na namna anavyolitazama suala la kiwakati pamoja na kubainisha athari za mitazamo hiyo kwa jamii.

## Methodolojia ya Utafiti

Data za utafiti huu zilipatikana maktabani na uwandani. Mtafiti alitumia mbinu ya kusimbisha maudhui katika uchanganuzi wa data. Data zilipangwa kwa kuzingatia mfanano wa kimaudhui na kisha kuwasilishwa kama matokeo ya utafiti, kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Matini zilizochambuliwa ni riwaya tatu za Kiswahili; *Bina - Adamu* (Wamitila, 2002), *Babu Alipofufuka* (Khamis, 2001) na *Nagona* (Kezilahabi, 1990). Riwaya hizi zilichaguliwa kama kiwakilishi cha kazi za fasihi ambazo maudhui yake yameibeba Falsafa ya Kiafrika, ambayo ndiyo kiini cha mada ya utafiti. Kwa upande mwingine, data za uwandani zilikusanywa kwa kuwasaili wataalamu na wanafunzi wanaojihusisha na masuala ya Fasihi na Falsafa ya Kiafrika kutoka Idara ya Kiswahili, Idara ya Lugha za Kigeni na Fasihi pamoja na Wanafunzi wa Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu Cha Dodoma. Watafitiwa hawa walipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa wa kipekee. Katika aina hii ya usampulishaji, mtafiti huchagua watafitiwa wake kutokana na sifa za kipekee walizonazo katika kukidhi malengo ya utafiti (Ponera, 2019). Lengo la kujumuisha data za maktabani na uwandani ni kupata uthabiti wa matokeo ya utafiti. Aidha, makala imejadili mtazamo wa kifalsafa kuhusu Waafrika pekee na siyo kuhusianisha au kulinganisha na falsafa za jamii nyinginezo duniani.

## Matokeo ya Utafiti

Mjadala katika sehemu hii unabainisha namna mtazamo kuhusu wakati unavyojibainisha kupitia vipengele vinavyoibua falsafa ya Waafrika. Aidha,

kwa kuzingatia Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika kuwa maisha ya Mwafrika yanakitwa katika msingi mkuu wa 'kuwapo' kwa kitu au watu, utafiti uliozalisha makala hii umebaini kuwa, dhana ya 'kuwako' hudhihirika katika vipengele mbalimbali ambavyo ndivyo huibua maarifa ya Kifalsafa ya Waafrika. Baadhi ya vipengele hivyo, kama ambavyo vimekusudiwa kujadiliwa katika mjadala wa makala hii, ni suala la uzazi, malezi, uhai na kifo pamoja na busara na hekima.

**Uzazi**

Waafrika wanathamini sana suala la uzazi. Kwao, uzazi ndiyo njia inayoipa jamii uzima wa milele na sababu ya maisha kuendelea kuwapo (Magesa, 1998; Mbiti, 2011; na Kajosi 2013). Kama Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika inavyotuelekeza kuwa kuwapo kwa kitu au mtu kunaelezwa katika vipindi mbalimbali vya kinyakati ambavyo vina sifa ya kutambuana na kuathiriana, msingi huu umesaidia kubaini suala la uzazi kama kipengele muhimu kinachobainisha kuwapo kwa mtu. Pia, kwa kuzingatia msingi huu, imebainika kuwa Waafrika hulitazama suala la uzazi kama kiunganishi cha vizazi mbalimbali katika hali ya kuathiriana kwa vipindi mbalimbali vya kinyakati. Vipindi hivyo ni wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao. Hii ina maana kuwa uzazi ni njia pekee inayoweza kuwafanya wanajamii kumkumbuka mtu aliyekufa kwa kuirejelea zamani kwani atakuwa ameacha kumbukumbu ya kudumu (mtoto). Pia, kupitia uzazi, huwafanya wanajamii kuitazama zamani kwa kuwahuisha wahenga na kuwaunganisha katika vizazi vilivyopo na vijavyo (Mbiti, 2011). Naye Faustine (2017), anafafanua kuwa suala la uzazi katika jamii za Kiafrika linatazamwa katika duara la mwendelezo usiokwisha. Mwisho wa uzao mmoja ndio mwanzo wa uzao mwingine ambao unadhihirisha tulikotoka, tulipo na tunapokwenda. Kimsingi, mtazamo huu wa Faustine (2017) unajenga picha

ya jumla kwa namna Waafrika wanavyoutazama wakati katika ncha tatu. Zamani (jana) ndiyo inayoweka misingi ya kuiishi sasa (leo) na sasa inafanya maandalizi ya kuiishi kesho itarajiwayo. Naye Duwe (2020)[1] anasema kuwa: "Uzazi katika jamii yetu una thamani kubwa sana. Unajua mimba ni jana, mtoto ni leo na anatarajiwa kuwa mzazi ambaye atawakilisha kesho." Mtazamo wa mtafitiwa huyu kuhusu Waafrika kuitazamia kesho unakinzana na ule anaoutoa Sanga (2020)[2] anayesema:

> Waafrika wana jana na leo na kesho hawaitilii maanani. Kwa mfano utoaji wa majina ya waliokufa, matambiko na mambo mengineyo yanaidhihirisha leo na kwa lengo la kuwakumbuka waliopita. Suala la wakati kwa Waafrika linatazamwa katika duara kwa maana ya kuwa jana na leo vinahusiana. Bila jana leo haipo. Mtazamo wa uzazi kuhusu kesho nadhani ni katika kuijenga leo itarajiwayo ambayo haijatimia kwani kesho haiwezi kuwa katika utimilifu. Pale inapotimilika, na kwa vile Waafrika wanautazamia wakati katika utimilifu wa mambo, hiyo huwa siyo kesho tena bali ni leo.

Maelezo ya mtafitiwa huyu yanashabihiana na yale yaliyotolewa na Mbiti (2011) ambaye pia anafafanua kuwa Waafrika wanautazama wakati katika uduara. Hata hivyo, mtafiti na mwandishi wa makala hii amebaini kuwa, pamoja na mtafitiwa huyu kubainisha suala la wakati katika ncha mbili, bado anatoa dokezo la kuwapo kwa mtazamo wa kesho ambayo kwake iko katika hali ya udhahania tu. Jambo hili linanasibishwa na sentensi anayoitoa inayoeleza kuwa mtazamo wa uzazi kuhusu kesho ni katika kuijenga leo itarajiwayo ambayo haijatimia na haiwezi kuwa katika utimilifu. Pale inapotimilika, na kwa vile Waafrika wanautazamia wakati katika utimilifu

---

[1] Bi. Duwe alikuwa mwanafunzi na mtafiti wa Shahada ya Uzamivu, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

[2] Sanga ni Mhadhiri Mwandamizi na mtaalamu wa Fasihi ya Kiswahili, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

wa mambo, hiyo huwa siyo kesho tena bali ni leo. Mawazo haya yanabainisha wazi wazo la Waafrika katika kuifikiria kesho, na kwamba ina umuhimu mkubwa kwa namna wanavyoyaendesha maisha yao.

Katika riwaya ya *Bina - Adamu!* dhana ya wakati inadhihirika kupitia kipengele cha uzazi pale Babu anapoeleza kuhusu tukio la kuzaliwa kwa Bina Adamu Msafiri. Huyu anazaliwa akiwa na sifa sawa na za Jagina aliyefariki miaka mingi iliyopita, na kusadikiwa kuwa kuzaliwa kwake ni ujio wa Jagina (aliyekuwapo na kisha kufariki) kwa mara ya pili (Wamitila, 2002:58). Kama Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika inavyosema kuwa dhana ya kuwapo hujifungamanisha na vipindi mbalimbali vya kinyakati, kitendo cha kuzaliwa kwa Bina Adamu Msafiri ambacho kinadhihirisha suala la "kuwapo" kinaakisi mtazamo wa Waafrika kuhusu falsafa ya uzazi ambayo inajifungamanisha na suala la kiwakati. Waafrika hawautazami wakati katika upekee wake bali kwa kuuhusisha na vipengele vingine vinavyoathiri maisha yao. Kwa mantiki hiyo basi, Jagina anayezungumzwa kwenye riwaya hii ni kiunganishi cha wakati katika ncha tatu. Hii ina maana kuwa, katika zamani, anatazamwa kama ni kumbukumbu ya Jagina aliyekufa miaka mingi iliyopita. Katika sasa, ni mtoto aliyezaliwa kwa mara ya pili kama Bina Adamu Msafiri na kutoa matumaini katika jamii kama kiungo cha ndoa na kinachojenga umuhimu wa familia, na katika kesho, ni kiumbe anayetazamwa kama mlinzi na mrithi wa wazazi wake pindi watakapokuwa wazee.

Pia, katika riwaya ya *Nagona*, mtazamo kuhusu wakati kama kipengele kinachoibua Falsafa ya Waafrika unabainika kupitia tukio la kuzaliwa kwa Mkombozi wa Pili. Katika tukio hilo, mwandishi anadhihirisha wazi namna Waafrika wanavyoutazama wakati katika ncha tatu yaani zamani, sasa, na

kesho kupitia kinywa cha mama mjamzito pale anaposema: "… unaiona mimba hii! Basi ni ya mkombozi wa pili. … maelfu ya miaka niko hapa nikisubiri azaliwe …" (Kezilahabi, 1990:43). Kwa mujibu wa Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika kuwa dhana ya kuwapo hujibainisha katika vipengele mbalimbali ambavyo vina sifa ya kutambuana na kuathiriana, tunaona wazi namna mwandishi anavyolihusisha suala la wakati na uzazi kama vitu vinavyoathiriana. Maneno yanayozungumzwa na mama mjamzito kupitia suala la uzazi yanabainisha hali halisi kwa namna Waafrika wanavyoutazama wakati. Kwanza, ni pale anapoidokeza dhana ya mkombozi wa pili ambayo, kimsingi, inaashiria kuwapo kwa mkombozi wa kwanza anayewakilisha mtazamo kuhusu zamani ambaye ndiye sababu ya kuwapo kwa mkombozi wa pili. Kiashiria kingine kinachobainisha kuwa Waafrika wanautazama wakati kwa kuitazamia zamani ni neno maelfu ya miaka ambayo yametumika kusubiri kuzaliwa kwa mkombozi wa pili. Aidha, udhihirikaji wa mimba "… unaiona mimba hii! ..." ni kibainishi cha sasa anayoishi mama mjamzito; na matarajio ya kuzaliwa kwa mkombozi wa pili yanadhihirisha mtazamo wa wakati ujao ambayo ni kesho.

Kwa ujumla, suala la umuhimu wa uzazi ambalo linabainisha namna Waafrika wanavyoutazama na kuuthamini wakati kuhusu zamani, sasa na kesho, lina athari kubwa sana katika maisha ya Waafrika. Kwa kuithamini zamani, Waafrika huendelea kuthamini vizazi vilivyopita kwa maana ya wafu. Huu ndio msingi wa kuwathamini wahenga na kuendelea kuishi kwa kuwaheshimu kwa kuamini kuwa wana nafasi kubwa katika ustawi wa maisha yao. Waafrika hufanya matambiko na ibada mbalimbali kama njia ya kuendelea kuwaenzi na kuomba baraka kutoka kwa wahenga (Faustine, 2017). Athari nyingine ya kifalsafa inayotokana na mtazamo kuhusu wakati

kupitia kipengele cha uzazi ni namna Waafrika wanavyoishi ‘sasa’ kwa kuwathamini watoto kuwa ndio msingi wa maisha kwa wanajamii, na kuihofia kesho kwa kuweka matumaini kwa watoto kuwa ndio walinzi na wasaidizi wao wa baadaye. Waafrika wamekuwa wakilitazama suala la uzazi katika umuhimu mkubwa na kuona kuwa mtu mwenye uwezo wa kuzaa ni mwenye baraka na yule asiye na uwezo huo ni mwenye laana (Magesa, 1998; Mbiti, 2011; na Faustine, 2011). Jambo hili huthibitika pia kupitia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi. Kwa mfano, methali isemayo: “Asiye na mwana aeleke jiwe.” Methali hii bila shaka hukusudiwa kumbeza mwanamke asiyezaa kwa jamii za Waafrika.

**Malezi**

Suala la uzazi ni kipengele muhimu sana kinachobainisha mtazamo kuhusu falsafa ya wakati kwa Waafrika. Hata hivyo, kama Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika inavyoelekeza kuwa suala la kuwapo hudhihirika pia kupitia kategoria mbalimbali na mahusiano ya kategoria hizo, makala hii imebaini kuwa umuhimu wa mtoto hauishii tu katika kuzaliwa bali huhusisha pia suala la malezi. Kutokana na umuhimu wa mtoto kuwa ndio kiungo katika kuuendeleza ukoo, mlinzi na pia mrithi wa wazazi wake pindi watakapokufa (Magesa, 1998; Mbiti, 2011), Waafrika huwalea watoto wao kwa kuzingatia mtazamo wa kiwakati. Malezi yao hukitwa katika kuwaandaa watoto hao kwa ajili ya kuishi sasa kama fahari ya wazazi wao, kesho kama walinzi na warithi wa familia zao na kama kiunganishi kati ya vizazi vilivyopo na vilivyopita. Akizungumzia suala la mahusiano ya mtazamo wa wakati na vipengele vinavyoibua Falsafa ya Waafrika, Kilatu (2020)[3] anasema kuwa:

[3] Kilatu ni Mhadhiri na mtaalamu wa Fasihi kutoka Idara ya Lugha za Kigeni na Fasihi, Chuo Kikuu cha Dodoma.

> Katika jamii za Kiafrika, baada ya mtoto kuzaliwa, matarajio ya wazazi ni kumlea katika maadili mema kwa ajili ya maisha ya baadaye. Malezi haya huhusisha pia suala la kimaadili katika kujenga heshima kwa vizazi vyote; vilivyopita (wahenga), vilivyopo na vijavyo. Kwa maana hiyo Waafrika hawawezi kumlea mtoto kuiishi leo pasipo kumrejesha katika jana. Na leo anayoiishi inakusudiwa kumfanya kuwa mwanajamii bora wa baadaye. Kimsingi tunapoangalia suala hili la malezi kwa kina, tunaweza kuona wazi namna Waafrika wanavyoutafsiri wakati. Hii ina maana kuwa wanaitambua zamani kwa kuirejelea zamani, leo katika kuiishi sasa na pia kesho katika kuwaandaa vijana wao kwa maisha ya baadaye.

Mtazamo wa mtafitiwa huyu unakinzana na mawazo ya wanafalsafa wa Kimagharibi wanaoutazama wakati katika ncha mbili kwa kuamini kuwa Waafrika hawaithamini kesho kwani ni dhahania (Mbiti, 2011). Kilatu (2020) anabainisha wazi namna Waafrika wanavyoithamini kesho kupitia suala la malezi ya mtoto ambayo yanakitwa katika kumwandaa mtoto katika matarajio ya kuwa msaada mkubwa kwa wazazi wake hapo kesho. Aidha, anafafanua wazi kuwa, kwa Waafrika, malezi ya watoto hufanyika kwa kuirejelea jana ambapo humwekea mtoto misingi mizuri ya kimaadili, kuiishi leo na, hatimaye, maandalizi yanayowaweka katika matarajio ya kuiishi kesho ambayo yana maana kubwa sana katika kuukamilisha mzunguko wa maisha.

Dhana ya wakati, kwa kadri ya mtazamo wa Waafrika, inabainika pia katika riwaya ya *Nagona* kupitia malezi ya mhusika Mimi. Katika riwaya hiyo, Babu anamwandaa Mimi kuwa kiongozi kwa kumpa jukumu la kumsaka Paa kama njia ya kumwandaa katika kesho kwa kuirejesha zamani, kuitazamia sasa na kuitarajia kesho. Anawaambia wazee wamtengenezee Mimi uta kama maandalizi ya safari yake kwa kusema, "… mtengenezeeni

uta na mishale akamsake Paa aliyepotea karne nyingi zilizopita …" (Kezilahabi, 1990:17). Katika kuirejesha zamani, anamwambia mjukuu wake kuwa anatakiwa akamsake paa aliyekwishapotea miaka mingi iliyopita, na mwanzo wa safari yake ni lazima ampokee aliyekuwa na uta kwa maana kwamba ni lazima aanze pale zamani ilipokomea "… mwenye uta na mshale ndiye anayepokelewa …" (Kezilahabi, 1990:18). Suala hili linaonesha kuwa zamani ni kiunganishi muhimu katika kuiishi sasa ambapo katika sasa, Babu anadhihirisha kukua kwa Mimi kwa kusema: "kwa sasa umekuwa kijana mkubwa nataka wazee wakutengenezee uta mkubwa na mshale. Lakini hawatakupa wao wenyewe mkononi. Utavipata wakati fulani na mahali fulani" (Kezilahabi, 1990:20).

Kama ilivyo katika jamii nyingine duniani, suala la malezi lina umuhimu mkubwa kwa Waafrika. Matumaini ya mtoto, kama kiongozi, mrithi na mlezi wa familia kwa wakati ujao, yanakitwa katika misingi ya malezi bora. Waafrika wanaamini kuwa, kiongozi na mrithi bora wa familia anajengwa kutokana na asili yake inayokitwa katika chimbuko lake; yaani zamani, leo anayoiishi na kesho aitarajiayo. Huu ndio msingi kwa jamii kuwaandaa watoto na vijana kwa kuweka msisitizo katika malezi bora ambayo yanaijumuisha jamii nzima.

**Uhai na Kifo**

Kipengele kingine cha kifalsafa ambacho hubainisha mtazamo wa Waafrika kuhusu wakati ni suala la uhai na kifo. Miongoni mwa wataalamu waliozungumzia mtazamo kuhusu uhai na kifo kwa Waafrika ni Temples (1969), Marealle (2011), Mbiti (2011), na Faustine (2017) kwa kuwataja baadhi tu. Wataalamu hawa wamezungumzia suala hili kwa kulihusisha na dhana ya duara la maisha lisilokuwa na mwisho. Wanafafanua kuwa, kwa

Waafrika, mtu hafi jumla. Kifo ni mwanzo wa maisha mengine ya mwanadamu katika ulimwengu tunaoishi kama kiumbe kipya, au ni mwendelezo wa maisha katika ulimwengu wa wafu hai. Kwa upande mwingine, Mbiti (2011), anahusisha falsafa ya uhai na kifo na suala la wakati kwa kulitazama katika ncha mbili. Anautazama uwepo wa mwanadamu katika dhana ya 'sasa'; kwamba yupo katika wakati tuliopo, na kifo chake kama 'zamani' kwamba alikwishapita. Kwa mtazamo wa Mbiti, (2011), Waafrika hawaitilii maana kesho kwani iko katika hali dhahania na kwao si timilifu. Thomas (2020)[4] anafafanua dhana ya uhai na kifo kwa kuihusianisha na mtazamo kuhusu dhana ya wakati kwa kusema:

> Kwa Waafrika, mpaka unaotenganisha kifo na uhai ni finyu sana. Kama inavyoelezwa na Wataalamu kama Temples (1959) na Mbiti (2010), Waafrika wanaamini kuwa hakuna kifo kinachowatenga wanafamilia na jamii zao moja kwa moja. Mtu anapozaliwa huwa ametarajiwa kuwapo. Anapokuwapo, anaishi siyo kwa kurudi katika jana aliyotarajiwa bali katika matumaini ya kuifikia kesho. Anapokufa wanajamii huwa na matumaini ya kuendelea kuwapo kwake kwani wanaamini kuwa mtu huyo huendelea kuwapo kwa kuzaliwa upya au huendelea kuishi katika ulimwengu wa wafu hai. Wanafalsafa hawa wanaamini kuwa Waafrika wanayatilia maana maisha yao katika wakati uliopita na zamani. Lakini kiuhalisia, na kwa mtazamo wangu, kwao, kesho ina maana zaidi. Hii ni kwa sababu, wanaitumia zamani na sasa kwa ajili ya kujenga maisha yao ya kesho na siyo kurudi watokako. Ukiangalia mtazamo kuhusu duara la maisha kwa imani za Mwafrika, halizunguki katika leo na jana bali hutoka katika jana, huishi leo, na kuielekea kesho ambayo kuwapo kwake kumetokana na msingi uliowekwa katika jana na leo.

Kwa kuzingatia maelezo ya Thomas (2020), ni wazi kuwa kesho, kwa Waafrika, ina maana na athari kubwa katika maisha yao. Kesho itarajiwayo

[4] Thomas ni Mhadhiri Msaidizi ambaye ni mtaalamu wa Fasihi kutoka Idara ya Lugha za Kigeni na Fasihi, Chuo Kikuu cha Dodoma.

kwa Waafrika ndio msingi waushikao katika kuishi maisha yenye uadilifu katika 'sasa' waliyopo ili waweze kuwa na nafasi na maisha mazuri wanayoyatarajia 'kesho' katika ulimwengu wa wafu hai. Schott (2010) anasema kuwa mtu anazaliwa ili aweze kufa. Tishio la kifo linaanza mara baada ya kuzaliwa kwake. Hapa ndipo Mwafrika anapoanza kuihofia kesho yake na kumfanya aishi kwa uadilifu ili baada ya kifo, aweze kupata makao mema kule aendako kutokana na matendo aliyoyafanya wakati wa uhai wake. Kwa mitazamo ya wanafalsafa na mtafitiwa tajwa, ni dhahiri kuwa, kwa Waafrika, wakati unatazamwa katika ncha tatu ambapo jana ya Mwafrika ndiyo kiunganishi muhimu katika kuiishi leo na kuitarajia kesho. Kwa maana hiyo basi, Mwafrika haishi katika kuimakinikia leo ambayo inamrudisha jana bali huizingatia leo kwa ajili ya kuwa na maisha mazuri katika kesho yake.

Kifo na uhai, kama kibainishi cha falsafa ya wakati kwa jamii ya Waafrika, hudhihirika pia katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*. Mwandishi anatumia mitazamo ya Falsafa ya Kiafrika kujenga taswira ya maisha ya Mzuka ambaye ni babu yake K. Katika riwaya hiyo, maisha ya Mzuka yanakitwa katika nyakati tatu tofauti zinazoakisi imani ya Waafrika kuhusu suala la wakati. Hali hii inadhihirika pale ambapo anayaegemeza maisha ya Mzuka katika kizazi kilichopita ambacho kinaibainisha zamani, vilevile kutambulisha kuwapo kwake katika sasa. Pia, anabainisha matarajio ya kuendelea kuwapo kwake katika dhana ya kuwapo kwa mwendelezo wa maisha baada ya kifo. Anuani ya kitabu *Babu Alipofufuka* inaashiria urejelezi wa tukio la kuwapo, kufa na kisha kufufuka kwa mzuka. Aidha, dhana ya kuwapo na kufa inadokeza zamani ya kiwakati katika kipindi cha uhai wa babu kwa sababu, katika uhalisia, mtu hawezi kufa, na wala

kufufuka pasipo kuwapo. Pia, mwandishi anafafanua mtazamo huu kupitia kinywa cha Babu pale anapomweleza K. kuwa, kuwapo kwa mwanadamu, kupo katika uendelevu wa kiwakati usio na kikomo. Anasema:

> "… Sikiliza K …" Aliendelea yule mtu maiti. Mimi babu yako; na hii ni kweli. Ukitaka usitake. Nimefufuka kitambo … au tuseme roho zetu zimo katika duru ya wakati wa daima usiomalizika. Ndio kusema hatukufa. Hatufi, wala hatutakufa. Hupotea kwenye macho yenu tu. Kila baada ya mpito wa miaka lazima tuje kukuzindueni. Na kwa muda mrefu sasa, nimekuwa nikijaribu kukupata na kujaribu kukuingia ndani … (Khamis, 2001: 20.)

Maelezo katika nukuu hii yanabainisha wazi kuwa kwa Waafrika, wakati ni endelevu na haukitwi katika ukomo wa utimilifu wa matukio. Sentensi anayoitamka babu: "… nimefufuka kitambo" inaashiria mtazamo wa kiwakati katika muktadha wa yaliyopita, yaani zamani. Aidha, kuwapo katika: "duru ya wakati usiomalizika" inabainisha uendelevu wa kiwakati katika sasa inayokitwa katika hali ya kuendelea, kwa maana ya kibainishi cha matarajio ya kesho. Sentensi: "Ndio kusema hatukufa. Hatufi, wala hatutakufa. Hupotea kwenye macho yenu tu. Kila baada ya mpito wa miaka lazima tuje kukuzindueni." inabainisha imani ya Waafrika kuhusu kesho, yaani wakati ujao ikihusishwa na mtazamo wa kuwapo kwa maisha baada ya kifo.

Kimsingi, mtazamo wa kiwakati unaojumuisha maisha ya mwanadamu katika vizazi vilivyopita, vilivyopo na vijavyo katika dhana ya uhai na kifo, una athari kubwa kwa jamii ya Waafrika. Huu ndio msingi wa Waafrika kuyakita maisha yao katika uadilifu, kuheshimu mizimu na wahenga kwa matarajio ya kuishi maisha mazuri sasa, na katika ulimwengu wa wafu pindi wanapokufa.

**Busara na Hekima**

Waafrika wanaamini kuwa busara na hekima anakuwa nazo mtu kutokana na uwezo wake wa kufikiri, kuamua jambo na kutenda. Kwao, umri ni kigezo kitumikacho katika kupima busara na hekima alizo nazo mtu (Wiredu, 1980). Mtazamo huu unatokana na imani kuwa mtu mwenye umri mkubwa huwa na busara na hekima za kutosha zaidi ya mwenye umri mdogo kutokana na uzoefu wa maisha anaokuwa nao kwani huwa amepitia mambo mengi (Tempels, 1969; Mbiti 2011; na Faustine, 2017). Hata hivyo, kigezo hiki hakipimwi kwa wazee walio hai peke yao, bali hujumuisha pia wafu hai (Tempels, 1969). Utafiti huu umebaini kuwa falsafa ya wakati, kwa mujibu wa Waafrika, inajibainisha kupitia mtazamo kuhusu busara na hekima kwani hujumuisha vizazi vilivyopita ambavyo huwakilisha zamani, vilivyopo, vinavyowakilisha leo na maisha ya vizazi hivyo yatarajiwayo baada ya kifo. Akifafanua namna suala la busara na hekima linavyobainisha dhana ya muda kwa Waafrika, Khamis (2020)[5] anaeleza kuwa:

> Kwa Waafrika, kama tunavyoelezwa na (Mbiti, 2011), umri wa mtu ni kigezo kikubwa kupima busara na hekima alizonazo. Hata hivyo, busara hizo huaminika kuwapo kwa wazee walio hai na wale waliokwishakufa miaka mingi iliyopita (wahenga). Heshima ya uhenga na, kama mtu unayeheshimika katika jamii baada ya kufa, hutokana na namna mtu mwenyewe alivyoishi kwa uadilifu duniani na nafasi yake kwa jamii. Mtazamo huu huyaathiri sana maisha ya Waafrika kwa kuwafanya waishi kwa uadilifu na kutenda maisha yaliyo mema kwa kuitarajia kesho yao ambayo ni maisha baada ya kifo. Huwafanya wanajamii kuishi katika misingi ya kuheshimiana ili waweze kuwa katika nafasi nzuri ya kuheshimika na kukumbukwa hapo baadaye. Kimsingi, baadaye wanayoitarajia siyo sasa wala jana, bali ni kesho …, ukiangalia kwa makini, kesho ya Waafrika ina thamani kwani kila wanaloliishi leo ni kwa matarajio

[5] Khamis ni Mhadhiri na mtaalamu wa Fasihi kutoka Idara ya Lugha za Kigeni na Fasihi, Chuo Kikuu cha Dodoma.

> ya kesho. Tunapokuwa na wazee wenye busara na hekima katika jamii, ina maana tuna matarajio ya kuwapo kwa wahenga ambao pia hutazamwa kama walinzi wa vizazi vijavyo.

Mtazamo wa mtafitiwa huyu unashabihiana na ule tulioupata katika data za maktabani kupitia riwaya ya *Nagona* na *Babu Alipofufuka*. Mathalani, katika *Nagona* mwandishi anamchora Babu kama mzee anayetumia hekima na busara kuiasa jamii yake katika nyakati zote. Katika kipindi cha uhai wake ambacho kinatazamwa kuwa ni 'sasa' anamuasa mjukuu wake Mimi kutopenda kunung'unika na kutokata tamaa katika maisha kama njia ya kupata mafanikio. Anasema "… Utawakuta wanafanya jambo fulani. Wewe pia fanya kama wao bila kuuliza, bila manung'unuiko na usikate tamaa … (Kezilahabi, 1990:15). Pia, anaifafanua zamani ya babu ambayo inabainisha namna babu alivyotumia busara na hekima zake kama mzee aliyeaminika kijijini kupitia kinywa cha Mimi pale anapoeleza kuwa:

> Babu yangu alijulikana sana kijijini. Wazee wengi walifika mara nyingi jioni kuongea naye. Baadhi walifika kutafuta mawaidha kuhusu migogoro yao, wengine walifika tu kusikiliza hekima yake na masimulizi ya kihistoria ya wakati uliopita. Mara nyingi nilikaa karibu naye kusikiliza maongezi yake na wazee ingawa hapakuwa mahali pangu (Kezilahabi, 1990: 15).

Waafrika wanaamini kuwa wazee ni sehemu ya watu wanaotoa miongozo na maadili kwa kutumia hekima na busara hata pale wanapokufa. Katika muktadha huu, babu huyu anatarajiwa kuendelea kutumia busara na hekima zake kuwaadilisha wanajamii akiwa katika maisha yake mengine kwenye ulimwengu wa wafu. Imani hii inabainisha mtazamo wa kiwakati kwa Waafrika katika ncha tatu; yaani zamani inayowakilisha maisha ya wahenga waliotazamiwa kuwa na busara na hekima katika kipindi cha uhai wao, sasa

ambayo inahalisika katika kuishi kwao na kesho yenye matarajio ya baadaye katika maisha yao kwenye ulimwengu wa wafu hai.

## Hitimisho

Makala hii imejadili namna dhana ya wakati inavyodhihirika kupitia vipengele vinne vinavyoibua falsafa ya Waafrika. Vipengele hivyo ni suala la uzazi, malezi, uhai na kifo pamoja na busara na hekima. Kupitia vipengele hivyo, makala imebainisha kuwa, Waafrika wanautazama wakati katika ncha tatu ambazo ni jana, leo, na kesho. Kimsingi, tofauti na inavyofafanuliwa na Mbiti (2011) kuwa, kwa Waafrika, kesho haina maana kwani haiko katika utimilifu, makala hii imebainisha umuhimu wa kuitazamia kesho kwani msingi wa maisha ya Waafrika ni katika kuiishi kesho yao. Namna wanavyoyaendesha maisha yao katika kutilia umuhimu katika masuala malezi, uhai na kifo pamoja na busara na hekima ni kwa ajili ya kuwa na maisha mazuri katika kesho wanayoitarajia.

## Marejeleo

Babalola, F.S. & Alokan, A.O. (2013). African Concept of Time, a Social Reality in the Process of Change. *Journal of Education and Practice*, 4 (7), 143-147.

Carazzon, R. (2010). Birth of New Science: The History of Ontology from Suarez to Kant. Inapatikana katika www.ontology.co/history. Ilisomwa tarehe 22/11/2022.

Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu* (Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Coffey, P. (1918). *Ontology or the Theory of Being*. London: Green and Co.

Faustine, S. (2017). *Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili* (Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Gyekye, K. (1975). African Religions and Phylosophy by J. S. Mbiti. Book review, *Second Order*, 4, (1), 86-94.

Kajosi, S. (2013). *Suala la Uzazi katika Ontolojia ya Kibantu na Jinsi Lilivyojitokeza katika Riwaya za Kiswahili* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Kant, I. (1998). *Critique of Pure Reason*. Combridge: Combridge Universty Press.

Kaponda, G.J. (2018). *Ontolojia ya Kiafrika katika Mbolezi za Wanyasa* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (2006). Utandawazi, Kiswahili na Dhana ya Wakati. Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI 2005 (Toleo Maalumu), 165-172.

Khamis, S.A.M. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: The Jomo Kenyeta Foundation.

Magesa, L. (1998). *African Religion: The Moral Traditions of Abundant Life*. NY: Orbis Books.

Marava, M.J. (2015). African Philosophy on the Concept of Time and its Influence on the View of Death and After Death – A Zimbabwean Perspecties. *International Journal of Philosop hy and Theory,* 3 (2), 87-97.

Marealle I.P. (2002). *Maisha ya Mchaga Hapa Duniani na Akhera*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Mbiti, J. S. (2010). *Introduction to African Religion*. Kampala: East African Educational Publishers Ltd.

Mbiti, J.S. (2011). *African Religion and Philosophy*. Kampala: East African Educational Publishers Ltd.

Nnajiofor, G.O. (2016). Justification of the Concept of Time in Africa. *Ogirisi: a New Journal of African Studies, (*12), 253 - 281. Inapatikana katika https://www.researchgate.net/publication/305627665 . Ilisomwa tarehe 18/12/2022.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Reeve, C.D.C. (2016). *Aristotle: Metaphyics*. USA: Hackett Publishing Company Inc.

Schott, R.M. (2010). *Birth, Death and Femininity*: *Philosophies of Embodiment*. Bloomington: Indiana University Press.

Tempels, P. (1969). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wolff, C. (1962). *Ontology*. Frankfurt: Hildesheim.